# Ulinganishi wa Mzizi wa Vitenzi katika Lugha ya Kiswahili na Kiarabu.

▪Dr. Hadija Jilala * ▪ Dr. Abdalla M. Aghel** ▪ Dr. Salma Hamad ***

**▪ Ikisiri**

Makala hii imelenga kuchambua ulinganishaji wa mzizi wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Vitenzi vinavyochambuliwa katika makala hii ni vitenzi vikuu vya lugha husika. Katika uchambuzi huo, makala hii, kwanza imeeleza kwa muhutasari uhusiano uliopo baina ya lugha ya Kiswahili na Kiarabu kwa ujumla wake kisha kufafanua dhana ya vitenzi inavyojitokeza kwenye lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Sambamba na hilo makala imeeleza dhana ya mzizi na namna unavyojitokeza pamoja na aina zake kwa mifano. Nadharia ya Umbo Upeo iliyoasisiwa na Prince na Smolensky mwaka (1993) ndio iliyoongoza uchanganuzi wa data katika kuangalia mzizi wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Makala imebaini kwamba lugha ya Kiarabu na Kiswahili zinatofautiana sana katika utokeanji wa mzizi wa vitenzi. Hii ina maana kwamba mzizi wa vitenzi vya Kiswahili hutengana na mofimu tamati kama maumbo mawili yanayojitegemea wakati mzizi wa vitenzi vya Kiarabu huungana na mofimu tamati kama umbo moja. Hivyo makala imehitimisha kwa kusema kwamba kuna tofauti kubwa ya namna mzizi wa vitenzi vya lugha ya Kiswahili vinavyojitokeza na uundaji *wake* ukilinganisha na mzizi wa vitenzi vya lugha ya Kiarabu.

تهدف هذه المقالة الى تحليل الجذور الفعلية في اللغة السواحيلية واللغة العربية وإجراء عملية مقارنة بينهما والأفعال التي تم تحليلها في هذه المقالة هي الافعال الرئيسية للغة السواحيلية والعربية، وتوضح هذه المقالة العلاقة بين اللغة السواحيلية والعربية ثم تشرح مفهوم الأفعال والتركيبة الفعلية للغة السواحيلية واللغة العربية إلى جانب ذلك تشرح المقالة مفهوم الجذر الفعلي، واعتمدت المقالة في جمع تحليل البيانات على نظرية التحليل الفعلي التي أسسها برنس وسمولنسكي سنة 1993 . واشارت المقالة إلى أن الاختلاف الكبير في التركيبة الفعلية بين اللغتين مما يدل على أن اللغة السواحيلية ليست كما تدعى بعض الآراء بأن أصولها تعود إلى اللغة العربية .

* Associate Professor Department Of Linguistics And Literary Studies The Open University of Tanzania.
* * lecturer Department of Afro-Asian Languages College of languages Tripoli University.
*** Assistant Professor Department Of Linguistics And Literary Studies The Open University of Tanzania.

## Utangulizi

Makala hii inachunguza ulinganishaji wa mzizi wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Vitenzi vinavyochambuliwa katika utafiti huu ni vitenzi vikuu vya lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Mtafiti alichukua vitenzi vya Kiswahili na kisha kuvitafsiri vitenzi hivyo kwa lugha ya Kiarabu ili kufanikisha lengo la makala hii ambalo ni kufanya ulinganishaji wa mzizi wa vitenzi baina ya lugha hizo mbili.

Wataalamu wa lugha na isimu wamepishana kimtazamo kuhusiana na asili ya lugha ya Kiswahili na hivyo kuibua mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza ni ule unaodai kuwa Kiswahili kililetwa na wageni kutoka nje ya Afrika ikiwemo Waarabu (Lodhi, 2006) ilhali mtazamo wa pili ni ule unaodai kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu ila imeathiriwa na lugha nyingine kutokana na mwingiliano wa ndani na nje ya bara la Afrika (Kihore, 1984; Bosha, 1993). Mtazamo wa pili unaonyesha kwamba maneno ya mkopo katika lugha ya Kiswahili si kutoka lugha ya Kiarabu pekee bali yamo maneno ya Kiajemi, Kireno, Kijerumani, Kiingereza, hata lugha nyingine za Kibantu (Massamba na wenzake, 2001).

Kama ambavyo lugha huathiriana, pia Kiarabu kimeathiri lugha nyingine kama vile Kiajemi, Kiurdu, Kimalezia, Kiamaziga, Kiindonesia, na nyingine nyingi. Kwa maana hiyo, Makala hii inakubaliana na wataalamu wanaodai kuwa lugha ya Kiswahili na Kiarabu zimeathiriana kutokana na kuingiliana na si kuwa lugha ya Kiswahili imetokana na lugha ya Kiarabu. Hata hivyo, ili kuthibitisha hili makala hii inafanya uchunguzi linganishi wa mzizi wa vitenzi baina ya Kiswahili na Kiarabu ili kuona kama kuna kufanana ama kutofautiana.

Baadhi ya watafiti wanakiri kwamba Kiswahili kina idadi kubwa ya msamiati wenye asili ya lugha ya Kiarabu. Krum (1940) pia amebainisha sauti za Kiarabu katika Kiswahili ambayo ni kama vile sauti ‘kh’ > [x] ambayo imeleta maneno kama vile khabari /xabari/, khitilafu /xitilafu/, khatari / xatari/, khamsa /xamsa/, na khamsini /xamsini/. Hussein (1988) amebainisha maneno yenye asili ya Kiarabu ambayo ni thamani, thawabu, theluji, dhambi, dhoruba, dhuluma, gharama, ghanima, ghorofa, methali, sahibu, na rafiki. Mwita (2009) amebainisha maneno ya Kiarabu yaliyoingizwa katika Kiswahili ambayo ni asquf>asikofu, taab > taabu, ibn amm> binamu, hukm> hukumu, dhulm>dhulumu, hisāb> hesabu. Lodhi (2006) ameonesha ukopaji wa fonimu za Kiarabu katika Kiswahili mfano fonimu x na q, muunganiko wa irabu ‘ai’ na ‘ei’, muunganiko wa konsonanti ‘st’ na ‘sh’.

Pia Petzell, (2005) ametaja maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu kama tubu, shukuru, salimu, thamini, samehe. Hali hii inatoa taswira ya jumla kwamba lugha hizi mbili zinakaribiana au zinafanana kiasi cha kuibua mjadala wa kwamba lugha ya Kiswahili imetokana na Kiarabu. Hata hivyo, tukichunguza kwa ukaribu zaidi, tunabaini kuwa watafiti hao walijikita zaidi katika kuchunguza kategoria ya nomino na misamiati ili kuthibitisha hoja zao za kukaribiana kwa lugha hizi mbili.

Kwa ujumla hatuna pingamizi na mfanano huo wa kimsamiati, lakini tunajiuliza je hali ikoje katika kategoria ya vitenzi vya lugha hizi hususani katika maumbo ya mzizi wa vitenzi? Je, kuna kufanana na kutofautiana kwa kiwango kwenye mzizi wa vitenzi baina ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu? Maswali haya ndiyo yaliyomshawishi mtafiti kuandika Makala hii ili kuona jinsi mzizi wa vitenzi vyenye herufi moja unavofana na kutofautiana katika lugha ya Kiswahili na Kiarabu.

**Dhana ya Vitenzi katika Lugha ya Kiswahili na Kiarabu**

Vitenzi ni aina mojawapo ya aina ya maneno katika lugha. Wataalamu mbalimbali wamefafanua kuhusu fasili ya vitenzi. Kwa mujibu wa TUKI (1990) kitenzi ni neno ambalo huarifu tendo linalofanyika. Masamba na wenzake (2001) wanafasili kitenzi kama aina ya neno linalotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu. Habwe na Karanja (2004) wanafasili kitenzi kama aina ya neno linaloarifu jambo linalofanywa na mtu, mnyama au kitu kingine chochote. Aidha, Richards na wengine (1985) wanadai kuwa kitenzi ni neno ambalo hutokea kama njeo, hali, nafsi, idadi na dhamira katika kueleza tendo au hali. Kutokana na fasili za wataalamu hao, makala hii imefasili kitenzi kama neno linaloonyesha tendo au hali ya kutenda katika nomino. Kitenzi hubeba mambo muhimu ambayo ni tendo lenyewe linalotendeka, wakati tendo linapotendeka, hali ya kitenzi chenyewe, kauli ya kitenzi chenyewe na uyakinishi au ukanushi wa kitenzi chenyewe.

Vitenzi katika lugha ya Kiswahili vimegawanyika katika aina kuu tatu ambazo ni: vitenzi vikuu, vitenzi visaidizi na vitenzi vishirikishi (Masamba na wenzake, 2001). Vitenzi vikuu hubeba taarifa ya tendo, hali ya tendo na kauli ya tendo. Vyote hivi huundwa na mofimu zilizounda kitenzi. Vitenzi vikuu huwa na maana hata kama vikisimama peke yake, huweza kuonesha ukanushi na huundwa kwa mofimu mbalimbali. Kwa mfano neno anafundisha; taarifa ya tendo ni kuelimisha ambayo imeundwa na mofimu "fundisha"; hali ya tendo ni ya kuendelea ambayo imewasilishwa na mofimu "na" na kauli ya tendo ni ya kutenda ambayo imewasilishwa na mofimu "fundisha". Kitenzi

kisaidizi ni kitenzi ambacho husaidia kitenzi kikuu kukamilisha sentensi. Kitenzi kisaidizi hakiwezi kuwa na maana iwapo kitasimama peke yake. Hii ndio maana kinaitwa kitenzi kisaidizi kwani maana yake utaipata iwapo kitatumika na kitenzi kikuu. Mfano wa kitenzi kisaidizi ni alikuwa, alikwisha, angali, ingawa, kuja, kwisha na kadhalika. Kitenzi kisaidizi hujulisha njeo, hujulisha uyakinishi au ukanushi na huundwa na mofimu mbalimbali. Sifa za Kitenzi kisaidizi ni kwamba hakikamilishi taarifa, mara zote huambatana na kitenzi kikuu katika kutoa taarifa na hudokeza nyakati mbalimbali za kutendeka kwa tendo. Kitenzi kishirikishi ni kitenzi ambacho huonyesha umoja wa vitu katika hali au tabia au katika mazingira ya aina moja. Mfano wa vitenzi vishirikishi ni kama vile alikuwa, si, ni, ndiyo siyo na kadhalika. Kutokana na ufafanuzi huu makala hii imejikita zaidi katika vitenzi vikuu kutokana na kwamba ndivyo huweza kubeba mofimu mbalimbali na hivyo kuwa na maana hata kama vitasimama peke yake.

Katika lugha ya Kiarabu, kitenzi kinafafanuliwa kama tamko lolote linalojulisha tukio na zama zake, yaani wakati ambao tukio limetokea aidha katika hali ya uhalisia au ukanushi. Vitenzi vya lugha ya Kiarabu huathiriwa na hali za kiisimu kama vile njeo, ukanushi, nafsi, kauli na hali zingine za kiisimu kama amri na kugeuka katika maumbo mbalimbali (انطوان الدحداح 2011;1882نبيل راغب,). Aidha, katika lugha ya Kiarabu, kitenzi hakiwezi kutimia bila kutajwa kwa mtendaji pamoja na nafsi. Sambamba na hilo, vitenzi vya lugha ya Kiarabu huwa na kanuni maalumu itumikayo, kugeuza neno kutoka jengo moja kwenda majengo mbali mbali yenye maana tofauti tofauti mfano mtendaji, mtendewa, kudogesha, kukuza n.k. (2019ابراهيم شمس الدين).

Katika lugha ya Kiarabu, kuna aina mbili ya vitenzi ambayo ni vitenzi ambavyo vinahitaji mtendwa viitwavyo مُتَعَدِيْyaani Muta-addiy. Mfanoضربَ dakhala ameingia.ضَرَبَ زَيْدٌ عَلِيًا(amempiga Zaidi Ally) كتبkataba ameandika كَتَبَ زَيْدٌ الدُرْسَ ameandika Zaidi somo =فَتَحَ fataha amefunguaفَتَحَ زَيْدُ البَابَ amefungua Zaydi mlango. Utakuta vitendo hivyo vinaishia kwa mtendewa. Aina ya pili ni vitendo ambavyo havihitajii mtendwa bali vinaishia kwa mtendaji tu viitwavyo لازم Laazim. Mfano wa vitenzi hivyo niدَخَلَ dakhala ameingia. دَخَلَ زَيْدٌ فِي المَسْجِدِdakhala Zaydun fil masjidi ameingia Zaidi Msikitini. مَاتَ maataamekufa مَاتَ مَرِيْضٌ maata mariydhwun amekufa mgonjwa.=نام naama (amelala) نَامَ زَيْدُnaama Zaydun amelala Zaydu. Utakuta vitendo hivyo vinaishia kwa mtendaji tu na havifiki kwa mtendewa (2006غمبو حسن).

**Dhana ya Mzizi wa Vitenzi.**

Mzizi ni sehemu ya neno ambayo haibadiliki hata kama neno hilo

litafanyiwa uambishaji, ukanushi, unyambulishaji na kadhlika. Kuna aina mbili za mzizi ambazo ni mzizi asilia na mzizi mnyambuliko. **Mzizi asilia** ni ule ambao hutokana na kitenzi halisi na hubeba maana ya msingi ya neno. Rejea jedwali lifuatalo

| KITENZI | MZIZI |
|---|---|
| KULA | -L- |
| IBA | IB- |
| SOMA | SOM- |
| ANDIKA | ANDIK- |
| PIGA | PIG- |
| CHEZA | CHEZ- |
| IMBA | IMB- |
| RUKA | RUK- |
| KAMATA | KAMAT- |
| LAUMU | LAUM- |

**Mzizi mnyambuliko** ni ule unaotokana na mchakato wa mnyambuliko yaani neno linapatikana baada ya mchakato wa unyambulishaji. Rejea jedwali lifuatalo

| KITENZI | MZIZI ASILIA | UNYAMBULISHAJI | MZIZI MNYAMBULIKO |
|---|---|---|---|
| KULA | -L- | ALIVYOLIWA | -LIW- |
| IBA | IB- | IMEIBIWA | -IBIW- |
| SOMA | SOM- | AMESOMEWA | -SOMEW- |
| ANDIKA | ANDIK- | AMEANDIKIWA | -ANDIKIW- |
| PIGA | PIG- | WAMEPIGANA | -PIGAN- |
| CHEZA | CHEZ- | ALIICHEZEA | -CHEZE- |
| IMBA | IMB- | WAMEIMBIWA | -IMBIW- |
| RUKA | RUK- | RUKIANA | -RUKIAN- |
| KAMATA | KAMAT- | KAMATANA | -KAMATAN- |
| LAUMU | LAUM- | LAUMIWA | -LAUMIW- |

Katika utafiti huu, mzizi asilia na mzizi wa mnyambuliko yote imetumika katika mchakato wa uwasilishaji na uchambuzi wa data. Data zilizochambuliwa

zimegawanywa katika makundi matatu ambayo ni mzizi wa vitenzi vya herufi moja, mzizi wa vitenzi vilivyoanza na irabu na mzizi wa vitenzi vilivyoanza na konsonanti.

**Kiunzi cha Nadharia**

Makala hii inaongozwa na Nadharia ya Umbo Upeo (NAUU) iliyoasisiwa na Prince na Smolensky (1993). Katika mwaka huo huo wa 1993 nadharia hii ilipanuliwa na kuendelezwa na McCarthy na Prince (Massamba, 2011). Lengo kuu la kuanzishwa kwa nadharia hii ni kupunguza udhahania uliokithiri wa uwakilishi wa vipengele vya kifonolojia katika kulikokotoa umbo la ndani kutoka umbo la nje kwa kutumia sheria na kanuni.

Katika muktadha huo, NAUU awali ilianzishwa ili kutatua matatizo ya kifonolojia lakini baadaye ikapanuliwa kwa kushughulikia masuala ya vipengele vingine vya kiisimu kama vile mofolojia na sintaksia (Massamba, 2011).

Mambo ya msingi yanayodaiwa na Nadharia ya Umbo Upeo (NAUU) ni kwamba miundo mbalimbali ya lugha hutokana na mwilingiliano baina ya mashartizuizi yanayokinzana. Mambo hayo yameegemezwa katika imani kwamba mfanano na utofautiano uliopo kati ya lugha moja na nyingine hutokana na tofauti za uthamini wa mashartizuizi yanayohusu mpangilio wa sauti, mofimu, maneno na virai. Watetezi wa nadharia hii wanaeleza kwamba mashartizuizi hayo ni ya kimajumui kwa maana kwamba yanapatikana katika lugha zote. Lakini upangiliaji wa mashartizuizi hayo hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine na kusababisha tofauti za sarufi za lugha mbalimbali.

NAUU imejengwa katika misingi mitatu ambapo msingi wa kwanza unaitwa zalishi (ZALI), msingi wa pili unajulikana kama mashartizuizi (MASHA -ZU) na msingi wa tatu ni tathmini (TATHI). Maelezo yafuatayo yanaelezea moja baada ya nyingine.

**Zalishi-**Huu ni msingi wa kwanza wa nadharia ya Umbo Upeo ambao kazi yake ni kuzalisha maumbo mbalimbali katika lugha inayohusika. Msingi huu huzalisha maumbo mbalimbali katika lugha lengwa ambayo kwa wakati mwingine huitwa maumbo shindani. Maumbo haya huitwa maumbo shindani kwa sababu ndiyo maumbo ambayo hufikia upeo wa ukubalifu. Na ikumbukwe kuwa umbo ambalo linafikia upeo ndilo umbo ambalo halikuvunja masharti katika lugha lengwa.

**Mashartizuizi-**Huu ni msingi wa pili; msingi huu huhusisha vigezo na masharti yanayoweza kukiukwa katika uzalishaji wa maumbo yasiyo weza kuvunjwa na yanayoweza kuvunjwa. Huu ni msingi ambao huamua ni umbo

lipi litafikia ukubalifu katika lugha husika. Hivyo basi lile umbo ambalo ama halikuvunja masharti yoyote au ambalo limevunja masharti yanayovumilika ndilo lipewalo ushindi (Massamba, 2011:250) kama inavyoonekana katika msingi wa tatu hapo chini.

**Tathmini-**Msingi wa tatu ni tathmini ambao huchagua umbo lililofikia upeo wa ukubalifu. Hiki ni kipengele muhimu sana kwani ndicho kinachoamua ni umbo lipi kati ya maumbo tokeo yaliyopo limefikia upeo wa ukubalifu. TATHI huangalia ni memba yupi katika jumla ya washindani kavunja masharti muhimu mengi kuliko wengine, yupi kavunja kidogo na yupi kavunja mengi zaidi katika upangiliaji. Hivyo basi kwa ujumla wake, nadharia hii ya NAUU huchukulia kwamba misingi hii mitatu hujitokeza katika kila lugha miongoni mwa lugha zilizopo ulimwenguni.

Nadharia hii imeteuliwa kutokana na sababu kwamba inauwezo wa kukidhi lengo la makala hii ambalo ni kulinganisha mzizi wa vitenzi vya Kiswahili na Kiarabu. Tuangalie data ifuatayo namna nadharia hii inavyotumika :

a. a-ta-ku-j-a

b. a-te-ku-j-a*

c. a-fa-ku-j-a*

Kwa kuangalia mfano hapo juu, tunaona kuwa masharti zuizi yanazuia kuwepo kwa silabi /fa/na /te/ kuonyesha njeo ya wakati ujao katika lugha ya Kiswahili. Hapa masharti zuizi ya utengamano hayakubaliki kutamka silabi zilizoandikwa hapo juu na kuleta maana. Hivyovivyo, katika mifano hapo juu, (rej 1b, c) maneno haya yamevuja masharti zuizi ya SI (shariti zuizi linalo zuia mabadiliko ya sifa, yaani kuwe na mshabaha wa sifa ya matamshi baina ya maumbo ghafi (MG) na maumbo tokeo (MT)). Hivyo basi kwa kurejelea mfano huo hapo juu, hii ina maana ya kwamba mahali pakutamkia sio penyewe ndio maana mtamkaji ametamka herufi zilizo sehemu hiyo na kuacha penye herufi kubalifu.

Sambamba na ukiukwaji wa masharti zuizi (MASHA-ZU), tunona pia kuwa msingi wa tathmini kama mojawapo ya msingi wa nadharia ya Umbo Upeo (NAUU) imeruhusu kutathmini (TATHI) umbo linalokubalika ambalo ni umbo (a) kama ilivyo onyeshwa hapo juu, hivyo basi /ta/ ndio umbo kubalifu linalo onesha njeo ya wakati ujao katika lugha ya Kiswahili.

Kwa ujumla, nadharia hii imetumika katika makala hii kulingana na utendaji kazi wa misingi yake katika lugha zitakazochunguzwa. Msingi wa zalishi ulitumika kuzalisha maumbo mbalimbali ya mofimu vya uambishaji

na unyambulishaji wa vitenzi vya lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Msingi wa mashartizuizi ulitumika kuchunguza vigezo na masharti ya utokeaji wa mofimu kwa utaratibu wa mofolojia ya lugha inayohusika. Na msingi wa tathmini ulisaidia kuchagua mofimu vinavyokubalika katika umbo la kitenzi cha lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Kwa mantiki hiyo, NAUU ni muhimu katika utafiti huu.

**Ukusanyaji Data**

Makala hii imetumia njia ya usomaji wa machapisho, dodoso na usaili ili kupata data zinazotakiwa.

Baada ya upatikanaji wa data mtafiti alitumia sampuli ya kinasibu kuchagua vitenzi vitakavyochanganuliwa na kisha mtafiti alipanga vitenzi hivyo katika kategoria kulingana na sifa, tabia na umbo la vitenzi. Vitenzi vinavyofanana kwa sifa, tabia na umbo viliwekwa katika kundi moja. Kwa kufanya hivyo tuliweza kupata mafungu matatu (3) ya vitenzi ambavyo ni; vitenzi vya herufi moja, vitenzi vinavyoanza na irabu pamoja na vitenzi vinavyoanza na konsonanti. Lugha ya Kiswahili ilikuwa ndiyo msingi wa ukusanyaji wa data ya vitenzi ambapo mtafiti alichukua vitenzi vya Kiswahili na kisha kuvitafsiri vitenzi hivyo kwa lugha ya Kiarabu ili kufanikisha lengo la makala hii ambalo ni ulinganishaji baina ya lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Kwa vile mtafiti ni mmilisi wa lugha ya Kiarabu kazi ya kutafsiri vitenzi vya Kiswahili kwa Kiarabu aliifanya yeye mwenyewe na pia kwa kusaidiana na baadhi ya watafitiwa wanaojua lugha zote mbili yaani Kiswahili na Kiarabu.

Mbinu ya dodoso na usaili zilitumika kupata data za ulinganishaji wa mizizi ya vitenzi vikuu vya Kiswahili na Kiarabu. Aidha, watafitiwa katika dodoso walionesha namna vitenzi vikuu vya Kiswahili na Kiarabu vinavyofanana na kutofautiana. Majibu ya usaili yalisaidia kupata ufafanuzi na maelezo zaidi kuhusu kufanana na kutofautiana kwa mzizi wa vitenzi vikuu vya Kiswahili na Kiarabu.

**Uchambuzi wa data**

Ili kuweza kufanya ulinganishaji wa mzizi wa vitenzi vya Kiswahili na kiarabu, makala hii imegawanya data katika makundi matatu ambayo ni mzizi wa vitenzi vya herufi moja, mzizi wa vitenzi vinavyoanza na irabu pamoja na mzizi wa vitenzi vinavyoanza na konsonanti.

***Mzizi wa Vitenzi vya Herufi Moja***

Vitenzi vya herufi moja ni vitenzi vilivyoundwa na herufi moja pekee ili kuleta maana. Mara nyingi vitenzi hivi huambatana na kiungo cha silabi KU-

ambacho hujitokeza mwanzoni mwa neno katika kauli ya kutenda ili kuleta maana kamili. Sifa nyingine ya vitenzi vyenye herufi moja ni kutosimama peke yake na kuleta maana. Aidha huweza kunyambuliwa kama ilivyo katika vitenzi vingine japokuwa mzizi wake hubaki sauti fulani kama ambvyo mzizi wa neno asilia ulivyokuwa. Mfano wa vitenzi vya herufi moja ni kufa, kula, kunywa, kunya, kuja n.k. Kwa mfano neno kula likinyambuliwa linakuwa ku- l- a; yaani dhima za kila mofimu zilizonyambuliwa huwa ni kama ifuatavyo:

- Mofimu "ku" huwasilisha mofimu ya herufi moja,
- Mofimu "l" ni mzizi wa neno na
- Mofimu "a" ni kiambishi tamati

Makala hii ililinganisha mizizi ya vitenzi vyenye herufi moja vya lugha ya Kiswahili na Kiarabu kwa kutumia maneno matatu ambayo ni kula, kunywa na kunya. Maneno haya yalitumika kama sampuli inayowakilisha vitenzi vingine vyenye herufi moja. Matokeo ya utafiti huu ni kama yanavyowasilishwa katika jedwali namba

**Jedwali 1. Mzizi wa Vitenzi vyenye Herufi Moja**

| NENO | LUGHA | RUWAZA |
|---|---|---|
| Kula | Kiswahili | SW: Ku (MFSB) → l (M) →a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: كُلْ→ (M)<br>KR2: kul → (M) |
| Kunywa | Kiswahili | SW: Ku (MFSBI) → nyw (M) → a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: إ (MFA) →شْرَبْ(M)<br>KR2: I (MFA) →shrab (M) |
| Kunya | Kiswahili | SW: ku (MFSB)→ny (M)→ a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: تَ(MFA) → غَوَّطْ→ (M)<br>KR2: ta (MFA) → ghawwatw → (M) |

Jedwari namba 1 hapo juu yanawasilisha matokeo ya ulinganishaji wa vitenzi vyenye herufi. Utafiti huu ulibaini kuwa vitenzi vinavyoundwa na mzizi wa herufi moja katika lugha ya Kiswahili vinajengwa na mofimu 'ku', ambayo haijitokezi katika lugha ya Kiarabu. Vilevile katika lugha ya Kiarabu mzizi wa neno hauwezi kuundwa kwa herufi moja kama ilivyojitokeza katika lugha ya Kiswahili (Rejea jedwari 1). Hii inadhihirisha kuwa kuna tofauti ya umbo la mzizi wa vitenzi vyenye herufi moja katika lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Hivyo basi, vitenzi

vilivyoundwa na mzizi wa herufi moja haviwezi kuwa na mfanano wowote kwenye lugha ya Kiswahili na Kiarabu. Hii inadhibitisha kile kilichosemwa na nadharia ya Umboupeo katika mhimili wake wa masharti zuizi kuwa kila lugha ina masharti na vigezo pekee yaani lugha ya Kiswahili na Kiarabu vina masharti zuizi katika muundo wa kauli kwenye vitenzi.

### *Mzizi wa Vitenzi Vilivyoanza na Irabu*

Vitenzi vinavyoanza na irabu ni kundi jingine la vitenzi ambalo utafiti huu umetumia katika ulinganishaji wake. Hivi ni vitenzi vyote vinavyoanza na irabu ambazo ni a, e, i, o, u. Katika kujadili ruwaza za vitenzi vinavyoanza na irabu utafiti huu ulibainisha makundi matatu ambayo yalidhihirishwa na data za utafiti huu. Makundi hayo ni kundi la ukanushi, wakati pamoja na nafsi pamoja. Matokeo yanajidhihirisha katika jedwali namba 4.3.

**Jedwali 2 Mzizi wa Vitenzi Vilivyoanza na Irabu**

| NENO | LUGHA | RUWAZA |
|---|---|---|
| Andika | Kiswahili | SW : Andik (M) →a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: أُ(MFA) → كْتُبْ(M).<br>KR2: u (MFA) → ktub (M) |
| Endesha | Kiswahili | SW: end (M)→ esh (MFSHZ)→a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: قْدْ (M).<br>KR2: qud (M). |
| Iga | Kiswahili | SW: Ig (M)→a (MFT). |
| | Kiarabu | KR1: ا(MFA) → قْتَدِ (M).<br>KR2: i → (MFA) قْتَدِ (M). |
| Oa | Kiswahili | SW: O (M)→a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: ا (MFA) → نْكَحْ (M).<br>KR2: i (MFA ) → nkah (M). |
| Ua | Kiswahili | SW: u (M)→a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: ا (MFA) →قْتُل (M)<br>KR2: u (MFA) → ktul (M) |

Ukichunguza jedwali namba 2 utabaini kuwa vitenzi vya Kiswahili vinavyoanza na irabu vina umbo la mzizi + Mofimu + Kiambishi tamati ambayo hukaa mwishoni mwa mzizi. Kwa upande mwingine, lugha ya Kiarabu katika vitenzi hivi vinavyoanza na irabu huanza na mofimu ya kiambishi awali + mzizi ambao unasimama ukiwa umefungamana na mofimu tamati kama umbo moja. Data hii ya mpangilio wa viambishi katika umbo la vitenzi vinavyaanza na irabu inadhihirisha kuwepo kwa tofauti baina ya Kiswahili na Kiarabu kama ilivyoelezwa kwenye nadharia ya Umbo Upeo katika mhimili wa masharti zuizi kwamba kila lugha huwa na vigezo na masharti ambayo huwaongoza watumiaji wa lugha hiyo katika uundaji wa maumbo sahihi ya maneno.

***Mzizi wa Vitenzi Vilivyoanza na Konsonanti***

Vitenzi vinavyoanza na konsonanti ni kundi jingine la vitenzi ambalo lilishughulikiwa katika utafiti huu. Hivi ni vitenzi vyote vinavyoanza na konsonanti zote za lugha ya Kiswahili. Vitenzi hivi vimegawanywa katika makundi mawili ambayo ni vitenzi vinavyoanza na konsonanti zenye silabi mbili na kundi la pili ni vitenzi vinavyoanza na konsonanti zaidi ya mbili.

**Jedwali 3 Mzizi wa Vitenzi Vilivyoanza na Konsonanti**

| NENO | LUGHA | RUWAZA |
|---|---|---|
| Toka | Kiswahili | SW: tok (M)→ a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: ا→ (MFA) → خْرُجْ(M)<br>KR2: u → (MFA) → khruj (M) |
| Pinda | Kiswahili | SW: pind (M) →a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: مِلْ(M)<br>KR2: mil (M) |
| Gonga | Kiswahili | SW: gong (M) → a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1:دَقَ (M)<br>KR2: daqqa (M) |
| Saka | Kiswahili | SW: Sak→ (M) →a(MFT) |
| | Kiarabu | KR1:ا (MFA) بْحَثْ (M)<br>KR2:I (MFA) bhath (M) |

| | | |
|---|---|---|
| Ficha | Kiswahili | SW: fich (M)→a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: أ (MFA) خف (M).<br>KR2: a (MFA) khfaa (M). |
| Funga | Kiswahili | SW: fung (M) →a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: أَ (MFA) غْلِقْ→ (M).<br>KR2: a (MFA) ghliq → (M). |
| Tegemea | Kiswahili | SW: tegeme (M) →a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: ا(MFA) → عْتَمَدْ(M).<br>KR2: I (MFA) → itamid (M) |
| Fafanua | Kiswahili | SW: fafanu (M) →a(MFT) |
| | Kiarabu | KR1: وَضِّحْ(M)<br>KR2: wadhwih (M) |
| Sumbua | Kiswahili | SW: sumbu (M)→a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: شَوِّشْ(M)<br>KR2; Shawwish (M) |
| Jaribu | Kiswahili | SW: jarib (M)→u (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: جَرِّبْ(M)<br>KR2: jarrib (M). |
| Kumbuka | Kiswahili | SW: kumbuk→ a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: ا (MFA) → ذْكُر (M)<br>KR2: u (MFA) →dhkur (M) |
| Maliza | Kiswahili | SW: maliz (M) → a (MFT) |
| | Kiarabu | KR1: أ(MFA) → كْمِلْ(M)<br>KR2: a (MFA) → kmil (M) |

Mifano katika jedwali 3 hapo juu inadhihirisha kwamba mzizi wa vitenzi vinavyoanza na konsonanti baina ya Kiswahili na Kiarabu umeonesha kuwa na tabia tofauti. Utafiti huu ulibaini kuwa katika lugha ya Kiswahili mzizi wa vitenzi hivi vinavyoanza na konsonanti hufuatana na mofimu tamati. Sifa hii ni tofauti katika lugha ya Kiarabu ambapo mzizi wa vitenzi hivi umeonesha kuwa unaweza kufuatana na mofimu awali ambayo hutokea mwanzoni au mzizi ukasimama peke yake kama umbo huru linalojitegemea pasipo kuzungukwa na maumbo mengine. Mpangilio huu wa mzizi wa vitenzi kama

unavyoonekana katika lugha ya Kiarabu hauwezi kukubalika katika lugha ya Kiswahili ambapo mzizi lazima uzungukwe na maumbo mengine. Hivyo basi utofauti huu unaonesha dhahiri kuwa lugha ya Kiswahili ni tofauti sana na lugha ya Kiarabu kama inavyosisitizwa katika mhimili wa masharti zuizi wa nadharia ya Umbo Upeo kwamba kila lugha huwa na masharti zuizi ambayo huwaongoza wazungumzaji katika kuunda maumbo sahihi ya maneno.

**Hitimisho**

Kutokana na makala hii, ni dhahiri kuwa Kiswahili kiliathiriwa tu na Kiarabu kwa sababu za muingiliano baina ya watu wa pwani ya Afrika Mashariki na Waarabu kama vile lugha zingine zilivyoathiriana kwa sababu za muingiliano. Madai ya kuwa Kiswahili kimetokana na Kiarabu yanaonekana kukosa mashiko hasa tukirejelea matokeo ya makala hii ambayo yanaonyesha utofauti mkubwa baina ya utokeaji na uundaji wa mzizi wa vitenzi vya Kiswaahili na Kiarabu. Utofauti huo umeonekana kkwamba mzizi wa vitenzi vya Kiswahili hutengana na mofimu tamati kama maumbo mawili yanayojitegemea wakati mzizi wa vitenzi vya Kiarabu huungana na mofimu tamati kama umbo moja.

**Marejeleo**

1- Bosha, I.A. (1993) *Taathari za Kiarabu katika Kiswahili, kamusi tathlitha Kiswahili Kiarabu na Kiingereza*. Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press.

2- Habwe, J. Na Karanja, P. (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi. Phoenix Publishers Limited

3- Hussein, A. (1988) *Ulinganishi wa Sauti za Kiarabu na Kiswahili*. Khartoum, Sudan: Khartoum International Institute of Arabic Language.

4- Kihore, Y.M. (1984) *Kiswahili katika Hati za Kiarabu katika Mulika 16*. Dar es Salaam: TUKI.

5- Krum, B. (1940) *Words of Oriental Origin in Swahili*. Northumberland Avenue W.C. 2: The Sheldon Press,

6- Lodhi, Y.A. (2006) *Verbal Extensions in Bantu*: The Case of Swahili and Nyamwezi

7- Massamba, D. P. B., Y. M. Kihore na J. I. Hokororo (2001) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA); Secondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

8- Mwita, C.M. (2009) *The Adaptation of Swahili Loanwords from Arabic: A Constraint Based Analysis*", ktk The Journal of Pan African Studies, Volume 2, number 8: 46-61

9- Petzell, M. (2005) *Expanding the Swahili vocabulary*: *Africa & Asia*. Sweden: Göteborg University Press.

10- Richards, J., Platt, J. na Weiber, H. (1985) *Longman Dictionary of Language and Teaching Applied Linguistics*. Edinburgh Gate: Pearson Education Ltd.

11- TUKI, (1990) *Kamusi ya Isimu ya Lugha*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

المراجع العربية :

1 – انطوان الدحداح، معجم تصريف الأفعال العربية، مكتبة لبنان للطباعة والنشر والتوزيع، بيروت، لبنان، 2011.

2 – نبيل راغب، القواعد الذهبية لإتقان اللغة العربية في النحو والصرف والبلاغة، دار راغب فرج للنشر والتوزيع والطباعة، بيروت، لبنان،1982 .

3 – إبراهيم شمس الدين، مرجع الطلاب في تصريف الأفعال، دار الكتب العالمية، بيروت، لبنان، 2019 .

4 – غمبو حسن، ظواهر تصريف الافعال، مؤسسة المختار للنشر والتوزيع، القاهرة، جمهورية مصر العربية، 2007.